# SEKTA YA UJENZI

## 1.0 UTANGULIZI:

Katika kipindi cha mwaka 1961 – 1973 kazi ya barabara zilikuwa zikifanywa Public Works Department. Zikifuatiwa na uanzishwaji wa Communication works (Kikosi cha mawasiliano).

- Vifaa na mitambo iliyotumika ilikuwa duni trekta na sululu.
- Hali ya kupitika kwa barabara ilikuwa ni mbaya sana.
- Katika barabara zilizounganisha Wilaya na Wilaya vikosi viliwekwa vya kudumu ikiwa ni Lipumba, Bruma na Kilosa.
- Palikuwepo na gari moja ya kupitia hizo barabara ili kubaini ubovu na sehemu korofi.
- Kuhusu ujenzi wa majengo ulifanywa na kikosi cha communication works.

## 2.0 BAADA YA UHURU

Sera na sheria zilizotumika baada ya uhuru katika kuongoza Taasisi ya Ujenzi:

**SERA**

- Kujenga na kukarabati majengo yote na barabara pamoja na madaraja ya muda na ya kudumu kwa kushirikiana na wadau wengine katika kulinda na kuendeleza miundo mbinu.

**SHERIA**

Sheria zilizoongoza Taasisi ya ujenzi (W)

- Wizara ilikuwa na majukumu yafuatayo;

(i) Kuanzisha sera ya barabara.

(ii) Kuunganisha na kusimamia utekelezaji wa uwekezaji wa programu za barabara.

(iii) Kuandaa miongozo, viwango na vielelezo pamoja na vipimo na ufuatiliaji wa utendaji wa miundombinu ya barabara.

(iv) Kuendeleza na kujenga uwezo wa sekta ya barabara na madaraja

(v) Kuendeleza sekta binafsi katika kukarabati na usimamizi wa barabara.

(vi) Kutekeleza na kuhakikisha usalama wa mazingira na watendaji wa kazi za barabara.

(vii) Mamlaka ya barabara itasimamia maendeleo, matengenezo ya barabara zote za Taifa na vitendea kazi vinavyohusiana na mamlaka hiyo.

(viii) Kutakuwepo na barabara kusanya ambazo zitaunganisha makao Makuu ya Wilaya na Makao Makuu ya Tarafa.

- Pia itaunganisha Makao Makuu ya Kata na Tarafa.
- Kuwepo kwa barabara za mijini katika Halmashauri zote.

(ix) Kutakuwepo na barabara lishia ambazo zitaunganisha na kukusanya Matawi yote katika nyumba za watumishi mbalimbali, Viwanda na sehemu za biashara.

(x) Pia patakuwepo na barabara za Vijiji ambazo zitaunganisha Kata zinginezo.

- Kutakuwepo na barabara za wananchi zitaunganisha mtaa na Kijiji.

**UJENZI WA MAJENGO**

- Kuhakikisha majengo yote yafuate taratibu zilizowekwa.
- Mkaguzi wa majengo atakagua na kusimamia ujenzi yote katika Halmashauri na sekta binafsi.
- Kutoa mwongozo na ushauri wa ujenzi wa majengo ya Serikali na majengo ya watu binafsi.
- Kuwa na mamlaka inayosimamia ujenzi wa majengo yote ya Serikali na ya Taasisi ambazo sio za kiserikali.

## 3.0 MABADILIKO NA MATUKIO KATIKA MFUMO WA SIASA, ULINZI NA UTAWALA

- Uanzishwaji wa Bodi mbalimbali za usimamizi wa ujenzi zikiwemo:

- Baraza la ujenzi la Taifa (NCC)
- Wakala wa majengo (TBA)
- Wakala wa barabara (TAN ROADS)
- Bodi ya wakandarasi CRB, ERB na AQSRB
- Utawala bora katika ngazi zote za serikali kuu na serikali za mitaa kuhusiana na shughuli zote za ujenzi wa majengo na miundo mbinu ya usafirishaji hasa ya barabara kwa upande wa ulinzi kufanikiwa kufungua barabara za mipakani ambazo zimesaidia ulinzi na usalama wa nchi kwa ujumla.
- Kurahisisha usafiri katika maeneo mengi ya muhimu ili kuboresha uchumi wa nchi yetu.
- Technologia imekua kwa kasi kubwa hasa utendaji wa kazi na utengenezaji wa miundombinu ya barabara imeboreshwa, ukilinganisha na kipindi cha nyuma ambapo matumizi ya nguvu kazi ya mikono ilitumika na vyanzo hafifu zilitumika.
- Jamii imeweza kunufaika na hali ya sasa kutokana na mabadiliko hayo ya Teknologia.

## 4.0 MAFANIKIO YALIYOPATIKANA/FURSA ZILIZOPO

- Huduma za jamii zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa.
- Ujenzi wa madaraja ya kudumu yapatayo 150.

- Barabara na majengo mengi yamekarabatiwa na kuwa katika hali nzuri ya kupitika na kutumika chini ya Taasisi ya Ujenzi (W)
- Ujenzi wa barabara za lami katika Makao Makuu ya Wilaya.

## 5.0 CHANGAMOTO

- Ukosefu wa fedha za kutosha kukamilisha miradi na kufanya matengenezo ya mara kwa mara ya barabara.
- Barabara nyingi bado za udongo.
- Kukosa fedha za kuongeza nyumba za watumishi wa Halmashauri.
- Fedha za usimamizi wa miradi ya Kata na Vijiji kutojitosheleza na kufanya miradi mingi kutopata ushauri wa mara kwa mara.
- Rasilimali watu, vifaa na mitambo hazijitoshelezi.
- Lazima ongezeko la kujenga uwezo ndani liwe la kutosha.

## 6.0 MATARAJIO YA TAASISI YA UJENZI KWA MIAKA 50 INAYOKUJA

(i) Kuanzisha mafunzo ya ufundi wa ujenzi wa barabara katika ngazi ya Wilaya katika Chuo cha Maendeleo Mbinga ili kuifanya jamii ishiriki katika uboreshaji mzima wa miundo mbinu ndani ya Halmashauri (Kwa

kutumia Tecknologia ya Kisasa). (Labour based Technology).

(ii) Kuimarisha kitengo cha mitambo kwa kujenga uwezo na kuweza kupata seti ya mitambo ya kutosha ili kukabili changamoto za ukosefu wa mitambo na vitendea kazi za ujenzi.

(iii) Kuweka sheria ndogondogo ambazo zitawabana wanaokiuka taratibu na matumizi ya miundombinu ya Halmashauri.

(iv) Kwa kutumia mapato ya ndani kujenga nyumba za watumishi wa Serikali kwa awamu ambazo zitawasaidia watumishi wapya kupata unafuu wa maisha.

(v) Kuimarisha na kuanzisha kitengo cha Takwimu ndani ya Idara na Mafunzo kwa wadau juu ya miundo mbinu ya barabara.

(vi) Kuongoza matengenezo ya barabara za lami, toka km 5.5 mpaka km 200 ifikapo miaka 50.

(vii) Uanzishaji wa wakala wa Barabara (W) ambayo itashughulikia suala la barabara na miundo mbinu.

(viii) Kushirikisha wadau na walisaidia katika kupanua miundo mbinu ya barabara.

(ix) Mafunzo na semina mbalimbali kwa wadau kuhusiana na matumizi ya barabara.

(x) Kuimarisha utendaji wenye ufanisi katika utekelezaji wa miradi.

(xi) Kutoa fursa kwa watumishi kujiendeleza kitaalam kufikia Shahada ya Uzamivu.
(xii) Mafunzo kwa vitendo kutokana na mabadiliko ya Tecknologia ya mawasiliano na miundo mbinu.
(xiii) Kuhamasisha sekta binafsi kuendesha shughuli za ujenzi wa miundo mbinu ya Barabara.
(xiv) Kuimarisha ubora wa kazi zote za ujenzi katika Taasisi yangu.
(xv) Kuongeza rasilimali watu, kuongeza ufanisi wa kazi.

Kuhakikisha barabara zinapatikana kwa kipindi chote cha mwaka kwa pande zote za Halmashauri